

Kupaa Mbinguni kwa Yesu Kristo

Nabii Eliya alipopaa mbinguni, mrithi wake Elisha alitamani sehemu maradufu ya nguvu ya Eliya. Sharti la kuipata ni la kuvutia: Elisha angeipata sehemu hiyo tu kama angemwona Eliya akipaa mbinguni. Kwa hiyo Elisha alikaza macho sana ili asiukose wakati huo wa kupaa. Hakuukosa, akawa shahidi wa tukio la kustaajabisha (2 Wafalme 2:9-14).

Hata leo inaweza kuwa muhimu vilevile tusikose kupaa kwa Bwana. Bila shaka kulitokea zamani, na hakuwezi tena kukosekana. Lakini maana ya kupaa kwa Yesu mbinguni haisisitizwi mara nyingi. Kuna nafasi yake muhimu katika historia ya wokovu, kama vile kusulubiwa na kufufuka.

Amechukuliwa juu katika utukufu

Siri ya utauwa, msingi wa imani, inayofunuliwa kwetu katika nafsi ya Kristo, inajumuisha kwamba YEYE alichukuliwa juu katika utukufu.

Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu: Mungu alidhihirishwa katika mwili, akajulikana kuwa na haki katika roho, akaonekana na malaika, akahubiriwa katika mataifa, akaaminiwa katika ulimwengu, akachukuliwa juu katika utukufu. 1 Timotheo 3:16

Si tu kwamba utukufu ndio mahali alipopaa kwenda. Kuingia kwake mbinguni kwote kulifunikwa na utukufu. Wingu la utukufu wa Mungu lilimpokea, likawa msafara wa kuingia kwake mbinguni.

Alichukuliwa juu, katika wingu:

Naye alipokwisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Matendo 1:9

Ninaamini kwamba kupaa huku kwa Bwana hakukuwa kwa kustaajabisha kidogo kuliko kule kwa Eliya. Ni Mwana wa Baba, aliyetimiza utume wake kwa kuyatoa maisha yake, ambaye sasa anaingia mbinguni, anapanda juu kuvikwa taji, ili apokewe na Mungu Baba. Kwa kupaa kwake kunaanza kutawazwa kwake kwenye kiti cha enzi. Yesu, Mnazareti aliyedharauliwa, mara moja baadaye anafanywa Bwana na Kristo. Sasa anaketi kwenye kiti cha enzi cha Baba. Mwanadamu, aliye Mwana wa Mungu, anaingia kama mwanadamu wa kwanza mbinguni, katika ukumbi wa kiti cha enzi cha Mungu, naye anapokelewa na kukaribishwa kwa heshima zote, shangwe na kustaajabiwa ambavyo baba anaweza kumpa mwanawe. Mbingu ni shahidi wa tukio hili la pekee, kurudi kwa Yesu katika ufalme wa mbinguni, alikotoka (Yohana 3:13; 6:62). Mwana anarudi nyumbani, naye anasema:

Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye. Na sasa, Baba, unitukuze mimi pamoja na nafsi yako, kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ulimwengu haujakuwako. Yohana 17:4-5

Hata kabla ya hapo tunamsikia akisema:

Basi alipokwisha kutoka nje, Yesu akasema: Sasa ametukuzwa Mwana wa Adamu, na Mungu ametukuzwa ndani yake. Ikiwa Mungu ametukuzwa ndani yake, Mungu naye atamtukuza ndani yake mwenyewe, na mara atamtukuza. Yohana 13:31-32

Kupaa mbinguni, kulikotokea siku 10 kabla ya sikukuu ya Pentekoste na siku 40 baada ya kufufuka kwake, kunahusiana kwa karibu na kutukuzwa kwake. Tunaweza kujichorea mbele ya macho yetu

furaha ya mbinguni, jinsi Bwana wetu, kama mtangulizi wetu, anavyopokelewa mbinguni.

Ushindi na shangwe ya ushindi

Kupaa mbinguni ni uthibitisho wa ushindi wake. Vita vimepiganwa, ushindi umepatikana. Na mbingu inamtaka arudi:

Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu. Marko 16:19

naye yuko mkono wa kuume wa Mungu, amekwisha kwenda mbinguni, malaika na mamlaka na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake. 1 Petro 3:22

Yeye aliyeshuka ndiye yeye aliyepaa juu sana kupita mbingu zote, ili avijaze vitu vyote. Waefeso 4:10

Ikiwa kufufuka kwake tayari kulikuwa uthibitisho wa ukombozi uliokamilika, basi kwa kuchukua nafasi ya heshima iliyo kuu kuliko zote ulimwenguni, imetiwa muhuri kwa mwisho kwamba Kristo wa Mungu ametimiza, naam amezidi, madai yote ya Mungu. Kwa hiari alishuka, akaishi kama sisi, akafa kifo cha mwenye dhambi kwa ajili ya wengine, akashuka hadi pande za chini za nchi.

Neno linazungumza mara kwa mara kuhusu kushuka kwake na kupanda kwake. Ni umbali huu usio na mwisho, kujinyenyekeza huku kusiko na mipaka, kulikohitajika ili kutimiza shauri la Mungu. Na kuinuliwa kwake baadaye ni kusiko na mipaka vilevile, juu sana na kwa utukufu kiasi ambacho mwanadamu yeyote asingeweza kufika kamwe. Na inashangaza mno kwamba, kwa sababu alijinyenyekeza hivyo, anatufungulia mbingu. Hakuifungua tu njia; sisi tayari sasa tumehamishwa pamoja naye huko ndani yake.

Heshima ya nafasi yake kwenye kiti cha enzi inaweza kupimwa tu na mtu anayehisi jinsi alivyojinyenyekeza chini sana.

Ili avijaze vitu vyote! Ni kana kwamba katika kila pembe ya mbingu jina lake linasomeka; kila kitu kimetiwa alama yake na kujazwa naye!

Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kuwa Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo. Matendo 2:36

Neno hili pia linaonyesha wazi upana wa kupaa kwake na kutukuzwa kwake katika historia ya wokovu. Upana wa kutukuzwa kwake una matokeo kwa ulimwengu wote. Nyumba ya Israeli inapoteza ukiritimba wake juu ya wokovu wa Mungu; ulimwengu wote unaweza kumjua Kristo Bwana, aliyetiwa mafuta na Mungu.

Ukombozi umekamilika!

Bila shaka ukombozi huu tayari umetiwa muhuri na Mungu katika ufufuo. Lakini hapa, dhidi ya mandhari ya dhabihu na huduma za agano la kale zisizokwisha kamwe, upekee na uhalali wa milele wa kujitoa kwake na wa thamani ya damu yake vinaunganishwa moja kwa moja na kuingia kwake katika patakatifu pa mbinguni.

wala si kwa {au: kupitia} damu ya mbuzi na ya ndama, bali kwa {au: kupitia} damu yake mwenyewe, aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele. Waebrania 9:12

Pale Golgotha alitoa damu yake, yaani maisha yake, na kwa namna ya kiroho akaingia Patakatifu pa Patakatifu kwa damu yake. Lakini katika andiko hili jambo la msingi ni kwamba aliingia mara moja tu, wala hakutoka tena kama kuhani mkuu, na kwamba aliketi mkono wa kuume wa Mungu. “Huduma” ya ukombozi imekamilika, Kristo ameketi kwenye kiti cha enzi.

Yeye ndiye chanzo, muumbaji wa wokovu wa milele. Ni nani awezaye kudai jambo hili la kushangaza, ni nani awezaye kusema amekamilisha jambo kama hili?

naye akiisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa wote wanaomtii, akasalimiwa {au: akaitwa} na Mungu kuwa Kuhani Mkuu kwa mfano wa Melkizedeki. Waebrania 5:9

Lakini ni yeye tu ambaye Mungu anamsalimu na kumkaribisha katika patakatifu pake, aketi kwenye kiti chake cha enzi, mahali pa juu kuliko pote palipopo. Ni salamu iliyoje! Mwana anarudi baada ya miaka 33! Naye anapewa jina la heshima “Kuhani Mkuu kwa mfano wa Melkizedeki”!

Maneno ya Baba kwake yanajumuisha neno hili: Uketi mkono wangu wa kuume, hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako! Zaburi 110:1

Je, ukombozi wa milele usioweza kupingwa ungekuwa umekamilika, kama asingepokelewa na Mungu kwa namna hii?

Anatuwakilisha mbinguni – wokovu duniani!

Ameipita katika mbingu. Huko ndiko kupaa kwake mbinguni, ambako ni sharti la kazi yake ya Kuhani Mkuu. Alipaa katika maandamano ya ushindi, akionwa na malaika wote.

Basi, kwa kuwa tuna kuhani mkuu aliye mkuu, aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu; kwa maana hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu, bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji. Waebrania 4:14-16

Yeye hatazami tu, kama sisi tunavyofanya mara nyingi; la, anaomba na kumsihi Mungu kwa ajili yetu, ili tusikate tamaa katika njia nyembamba iendayo utukufuni.

Kwa hiyo aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiiao Mungu kwa yeye, kwa kuwa yu hai sikuzote ili awaombee. {au: ili awawakilishe, ili aombe kwa ajili yao} Waebrania 7:25

Roho wa Mungu: maji yaliyo hai, msaidizi na nguvu kutoka juu

Sharti la Roho wa Mungu kutumwa duniani siku ya Pentekoste lilikuwa Kristo aliyepaa mbinguni na kutukuzwa!

Aniaminiye mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani ya tumbo lake. Na neno hilo alilinena katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja bado, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa bado. Yohana 7:38-39

Roho wa Mungu alipaswa kumshuhudia Kristo aliyetukuzwa, na kuufanya utukufu huu kuwa hai kwetu katika njia yetu kuelekea lengo – njia ambayo kwa nje haionyeshi wala kudokeza chochote cha utukufu

huu wa Kristo, ambao atatushirikisha na ambao tayari sasa ni mali yetu. Kwa maana hii tunaweza pia kusema juu ya nguvu kutoka juu, kiini na matokeo ya utukufu ulio juu.

Kwa kweli ni siri yetu kwamba Bwana wetu sasa ni Bwana wa utukufu, na kwamba tuko njiani kuingia katika utukufu huo huo. Anataka kutuonyesha utukufu wake, ambao Baba alimpa kwa sababu ya kazi yake aliyoikamilisha.

Siku ya Pentekoste Roho huyu alikuja, akawa nguvu kutoka juu kwa wanafunzi. Lakini kila mtu anajua kwamba siku hii, kwa njia ya Roho huyo, ikawa saa ya kuzaliwa kwa kanisa la Mungu:

Basi yeye, akiisha kutukuzwa kwa mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia. Kwa maana Daudi hakupanda mbinguni; lakini yeye mwenyewe asema: "Bwana alimwambia Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako." {Zaburi 110:1} Matendo 2:33-35

Siku hiyo wanafunzi wote walinyweshwa Roho mmoja na kuunganishwa na Kichwa kilicho mbinguni. Kichwa na mwili ni picha na uhalisi wa muungano wa ndani na usioweza kutenganishwa wa Kristo na kanisa. Na Kichwa kilipaswa kuwa Kristo aliyetukuzwa, si chini ya yule anayevijaza vyote katika vyote. Si Kristo aliyefufuka kabla ya kupaa kwake, alipokuwa bado duniani, bali yule ambaye wakati ujao ni wake, yule anayetaka kulishirikisha kanisa utukufu huu milele. Hatakuwa mahali popote tena bila kanisa kuwepo pamoja naye, kwa sababu kichwa na mwili haviwezi kutenganishwa.

Kwamba Yesu angewaacha wanafunzi, ilibidi kuwahuzunisha. Lakini Mwalimu anawaonyesha wazi – na sisi pia kupitia Agano Jipya lote – jinsi ilivyo muhimu na lazima kabisa kwamba yeye arudi. Katika utupu huo Roho wa Mungu angeingia, na kuwajaza, na kukaa ndani yao. Angekuja tena, katika Roho huyu, ambaye pia anaitwa Roho wa Kristo.

Lakini sasa ninakwenda zake kwa yeye aliyenipeleka; wala hakuna kati yenu aniulizaye: Unakwenda wapi? Lakini kwa sababu nimewaambia hayo, huzuni imeijaza mioyo yenu. Lakini mimi nawaambia iliyo kweli: Yawafaa ninyi mimi niondoke; kwa maana nisipoondoka, yule Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu. Yohana 16:5-7

YEYE anatuandalia kufika kwetu!

Kupaa mbinguni pia kunahusiana moja kwa moja na tumaini letu. Ilimbidi aende, ili atuandalie makao pale ambapo amekuwa daima pamoja na Baba. Anapashughulikia mahali hapo yeye mwenyewe, ili papate kutufaa. Hilo linamaanisha nini? Anatutakia mema sana; hatujui hata kidogo kile kinachotungoja!

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; kwa maana naenda kuwaandalia mahali. Na mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo. Yohana 14:2-3

Mlisikia ya kwamba mimi naliwaambia: Naenda zangu, tena naja kwenu. Kama mngalinipenda, mngalifurahi kwa sababu naenda kwa Baba; kwa kuwa Baba [yangu] ni mkuu kuliko mimi. Yohana 14:28

Mwokozi anatuacha hapa tuuone moyo wake. Alitaka kurudi nyumbani! Hakuwa nyumbani katika ulimwengu. Alikuwa mgeni, mtumishi aliyekaza fikira zake kwenye kazi aliyopewa. Lakini alitaka

nyumbani kwake kuwe pia nyumbani kwetu.

Kwa hiyo hatutakuwa nyumbani duniani, bali kwake. Sisi tuliokuwa wa dunia hapo zamani bila shaka hatutakosa mengi, hata kama mawazo kama hayo yanatujia mara kwa mara.

Yesu ametangulia mbele kama mtangulizi wetu, naye sasa yuko katika patakatifu – mahali palepale panapoelezwa kama nyumba ya Baba, ingawa bila shaka kwa upande mwingine.

Tumaini hilo tunalo kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, ifikayo hata ndani ya pazia; alimoingia Yesu kwa ajili yetu kama mtangulizi wetu, amekuwa kuhani mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki. Waebrania 6:19-20

Mtangulizi ana wafuasi, nao ni sisi. Yeye ndiye mwanzilishi na mkamilishaji wa imani. Tutamfuata katika njia ileile aliyoipita katika mbingu. Hata jambo la “kuchukuliwa” kwetu atalishughulikia yeye mwenyewe, sawasawa na kupanga makao yetu.

YEYE anaacha agizo!

Akawaambia: Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Marko 16:15

Ingekuwa kosa kutoyanukuu maneno haya ya Mwalimu katika dakika za kuagana kwake na wanafunzi. Agizo liko wazi. Ni Injili ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo (2 Wakorintho 4:6). Ni ujumbe wa wokovu wa milele, ambao kwa ajili yake Kristo alikufa, akafufuka na kupaa mbinguni. Na nafasi yake kwenye kiti cha enzi cha Mungu inatupa mamlaka ya kwenda. Si ujumbe wa mtu aliyeshindwa, aliyeishia msalabani. Ni ujumbe wa Mshindi, anayekuja tena, aliye hai!

YEYE anakuja tena!

Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni. Matendo 1:11

Atasimama juu ya mlima wa Mizeituni:

Na miguu yake itasimama siku hiyo juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki; na mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake, kuelekea mashariki na kuelekea magharibi, ukawa bonde kubwa sana; na nusu ya mlima itaondoka kuelekea kaskazini, na nusu yake nyingine kuelekea kusini. Zekaria 14:4

Sasa ameketi kwenye kiti cha enzi cha Baba. Kisha, atakapokuja, atatawala kwenye kiti chake cha enzi, ambacho miguuni pake adui zake wote watakuwa chini (Ufunuo 3:21).

Utukufu alio nao tayari sasa utaangaza kama jua!

Kwa hakika kama ilivyokuwepo siku ya kupaa kwake, ndivyo kwa hakika itakavyokuwepo siku ya kurudi kwake! Haya yote tutayashuhudia kwa karibu kabisa. Haleluya!